



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA  
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA



TANGAZO KWA UMMA

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoungwa kwa **Sheria Namba 10 ya Mwaka 2005** na Marekebisho **Kifungu cha 4 Sura ya 339 R.E. 2016**. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu 5 (a-j) cha Sheria hiyo ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Bodi inawatangazia kuwa inaendelea kupokea maombi ya leseni za **Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala** kwa **Msimu wa Mwaka 2024/2025**. Pamoja na mambo mengine, waombaji wote wazingatie kuwa na sifa kwa kuzingatia **Kifungu cha 18(2)** cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala. Mahitaji muhimu ya kila aina ya maombi ya leseni yameambatishwa katika tangazo hili.

Gharama za maombi na ukauguzi wa leseni za Mwendesha Ghala, Meneja Dhamana na Mkaguzi wa Ghala ni **20,000/=**.

Aidha, kwa mazao na bidhaa au biashara zenye mzunguko wa mwaka mzima, waombaji wanaoendelea wanaelekezwa kuwasilisha maombi mapema kabla muda wa leseni kumalizika; ili kuwezesha maombi kufanyiwa kazi sambamba na ukaguzi wa ghala kwa wakati. Hii itahusisha bidhaa kama vile kakao, nafaka, mazao jamii ya kunde, mazao ya viungo na mengine ambayo hayatajwa kwenye Jedwali hapo chini.

Bidhaa na mazao yenye misimu maalumu ambayo hutegemeana na kalenda za ushirika; mnaelekezwa kuwasilisha maombi kabla ya tarehe tajwa katika Jedwali hapo chini. Maombi yatakayowasilishwa zaidi ya tarehe tajwa; pamoja na 20,000/= ya ada, mwombaji atagharamia ukaguzi wa ghala husika kwa kuzingatia viwango vya Serikali.

N	Bidhaa	Tarehe ya Mwisho Bila Gharama za Ukaguzi	Tarehe ya Mwisho wa Maombi
1	Ufuta	30 Aprili 2024	17 Mei 2024
2	Mbaazi	30 Juni 2024	14 Juni 2024
3	Koroshu	31 Agosti 2024	9 Septemba 2024
4	Choroko	31 Disemba 2024	15 Januari 2025

Maombi yote yawasilishwe kupitia **info@wrrb.go.tz**; au kupitia **S.L.P. 2095, Mtaa wa Nyerere Kitalu Na.3, Kiwanja Na.23 Dodoma**; au kwa njia ya **kieletroniki**.

Bodi inawahimiza kukamilisha taratibu za maombi ya leseni kwa wakati ili kujiepusha na usumbufu wa aina yoyote unaoweza kujitokeza.

**NB:** Maombi ambayo hayatakuwa na viambatisho vinavyotakiwa au mapungufu yoyote hayatafanyiwa kazi.

Imetolewa,

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**10 Aprili 2024**

# Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Kuwasilisha Maombi ya Leseni ya Mwendesha Ghala

Kujaza **Fomu Namba 1** na kuwasilisha viambatisho muhimu kama vilivyoanishwa hapo chini

## 1. Nyaraka za Kampuni

- Nyaraka za usajili kutoka mamlaka husika;
- Makubaliano ya Wakurugenzi wa Kampuni inayoomba leseni kufanya biashara inayoombwa kwenye ghala husika sambamba na utayari wa kulipa ada, kuwa na kinga ya utendaji na kufanya kazi kwa mujibu wa viwango vinavyotolewa na Bodi;
- Picha za Wakurugenzi/Wanahisa zilizothibitishwa na Mwanasheria;
- Wasifu wa Wakurugenzi/Wanahisa uliothibitishwa na wanasheria;
- Mchoro wa ramani unaonesha mahala makao makuu ya ofisi za Mwombaji zilipo au kuainisha namba za longitudi na latitudi

## 2. Umiliki wa Ghala;

- Hati inayothibitisha kuwa Mwombaji anamiliki ghala husika au;
- Mkataba wa kupangishwa ghala husika kwa muda wote wa leseni;

## 3. Ukubwa/Ujazo wa Leseni

- Kuainisha ukubwa/ujazo wa ghala unaoweza kuhifadhi bidhaa inayoombewa leseni;
- Kuainisha kiasi cha ukubwa/ujazo anaomba leseni kwenye ghala husika

## 4. Nyaraka za Uthibiti Hatari Ghalani

- Bima ya moto inayokinga bidhaa inayoombewa leseni inayozingatia thamani ya bidhaa husika;
- Bima ya wizi inayokinga bidhaa inayoombewa leseni inayozingatia thamani ya bidhaa husika;
- Bima ya uaminifu wa wafanyakazi ghalani;

## 5. Maelezo kuhusu Ghala

- Fomu Namba 2** iliyozajwa kikamilifu;
- Mchoro wa ramani unaonesha mahali ghala linaloombewa leseni linapatikana au kuainisha namba za longitudi na latitudi;

## 6. Vifaa Muhimu vya Kupima Ubora Ghalani

- Uthibitisho wa **kipima unyevu** kilochohakikiwa na **Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**;
- Uthibitisho wa **mzani** uliohakikiwa na **Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA)**;
- Vifaa vingine muhimu kama chekeche ya maabara (*laboratory analysis sieve*), bambo ya kuchukulia sampuli kutoka kwenye vifungashio; vijiko vya maabara vinavyotosheleza mahitaji ya upimaji wa sampuli, bakuli za kupimia sampuli n.k

## 7. Taarifa zinazohusu Masuala ya Fedha;

- Barua ya uthibitisho wa akaunti ya Kampuni kutoka benki husika;
- Taarifa za fedha za Kampuni za karibuni;

## 8. Taarifa za Wafanyakazi wa Ghala

### a. **Meneja:**

- Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
- Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
- Wasifu
- Awe na angalua shahada ya kwanza
- Vyeti vya Taaluma
- Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

### b. **Karani wa Ubora:**

- Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
- Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
- Wasifu
- Awe na angalau diploma (inayohusu bidhaa atakayosimamia kilimo/ misitu n.k)
- Vyeti vya Taaluma
- Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

### c. **Karani wa Kumbukumbu:**

- Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
- Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
- Wasifu
- Awe na angalau diploma
- Vyeti vya Taaluma
- Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

### d. **Mtunza Stao:**

- Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
- Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
- Wasifu
- Awe na angalau elimu ya diploma
- Vyeti vya Taaluma
- Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

### e. **Karani wa Mzani:**

- Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
- Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
- Wasifu
- Awe na angalau elimu ya cheti
- Vyeti vya Taaluma
- Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

## 9. Gharama za maombi

- Mwombaji atalipa ada ya maombi **Tsh. 20,000/=**

## 10. Baada ya Kuwasilisha Maombi

- Ukaguzi wa ghala linaloombewa leseni na Afisa wa Bodi
- Kuweka **Kinga ya Utendaji** kwa kuzingatia masharti yatakayoinishwa baada ya maombi kuwasilishwa Bodi
- Endapo wafanyakazi hawana mafunzo ya WRRB watapaswa kushiriki, kufanya mtihani na kufaulu

# Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Kuwasilisha Maombi ya Leseni ya Meneja Dhamana

Kujaza **Fomu Namba 10** na kuwasilisha viambatisho muhimu kama vilivyopanishwa hapo chini

## 1. Nyaraka za Kampuni

- Nyaraka za usajili kutoka mamlaka husika;
- Makubaliano ya Wakurugenzi wa Kampuni inayoomba leseni kufanya biashara inayoombwa kwenye ghala husika sambamba na utayari wa kulipa ada, kuwa na kinga ya utendaji na kufanya kazi kwa mujibu wa viwango vinavyotolewa na Bodi;
- Picha za Wakurugenzi/Wanahisa zilizothibitishwa na Mwanasheria;
- Wasifu wa Wakurugenzi/Wanahisa uliothibitishwa na wanasheria;
- Mchoro wa ramani unaonesha mahala mako makuu ya ofisi za Mwombaji zilipo au kuainisha namba za longitudi na latitudi

## 2. Taarifa zinazohusu Masuala ya Fedha;

- Barua ya uthibitisho wa akaunti ya Kampuni kutoka benki husika;
- Taarifa za fedha za Kampuni za karibuni;

## 3. Umiliki wa Ghala;

- Hati inayothibitisha kuwa Mwombaji anamiliki ghala husika au;
- Mkataba wa kupangishwa ghala husika kwa muda wote wa leseni;

## 4. Ukubwa/Ujazo wa Leseni

- Kuainisha ukubwa/ujazo wa ghala unaoweza kuhifadhi bidhaa inayoombewa leseni;
- Kuainisha kiasi cha ukubwa/ujazo anaombea leseni kwenye ghala husika

## 5. Maelezo kuhusu Ghala

- Fomu Namba 2** iliyojazwa kikamilifu;
- Mchoro wa ramani unaonesha mahali ghala linaloombewa leseni linapatikana au kuainisha namba za longitudi na latitudi;

## 6. Nyaraka za Uthibiti Hatari Ghalani

- Bima ya moto inayokinga bidhaa inayoombewa leseni inayozingatia thamani ya bidhaa husika;
- Bima ya wizi inayokinga bidhaa inayoombewa leseni inayozingatia thamani ya bidhaa husika;
- Bima ya uaminifu wa wafanyakazi ghalani;

## 7. Vifaa Muhimu vya Kupima Ubora Ghalani

- Vifaa vya kupimia ubora wa bidhaa ili kuwezesha kupima ubora kama ilivyoelekezwa katika Kiwango cha Kitaifa cha bidhaa husika inayoombewa leseni;
- Vifaa hivyo lazima uwasilishwe uthibitisho vya kufanyiwa uhakiki na mamlaka husika kama vile Uthibitisho wa **kipima unyevu** kilochohakikiwa na **Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**, uthibitisho wa **mzani** uliohakikiwa na **Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA)** n.k.

## 8. Utaratibu wa Kazi/Mikataba ya Kazi

- Kuwasilisha mikataba/makubaliano ya utunzaji baina ya Mweka Mali, Meneja Dhamana na Benki,
- Au**, kuwasilisha mikataba/makubaliano ya utunzaji baina ya Mweka Mali, Meneja Dhamana na Mtoa Fedha
- Au**, kuwasilisha mikataba/makubaliano ya utunzaji baina ya Mweka Mali, Meneja Dhamana na Mtoa Huduma

## 9. Taarifa za Wafanyakazi wa Ghala

- Meneja:**
  - Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
  - Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
  - Wasifu
  - Awe na angalua shahada ya kwanza
  - Vyeti vya Taaluma
  - Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

### b. **Karani wa Kumbukumbu:**

- Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
- Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
- Wasifu
- Awe na angalau diploma
- Vyeti vya Taaluma
- Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

### c. **Karani wa Ubora:**

- Mkataba wa ajira wa muda usiopungua mwaka mmoja
- Picha iliyothibitishwa na Mwanasheria
- Wasifu
- Awe na angalau diploma (inayohusu bidhaa atakayosimamia kilimo/misitu n.k)
- Vyeti vya Taaluma
- Cheti cha Mafunzo yanayotolewa na WRRB

## 10. Gharama za maombi

- Mwombaji atalipa ada ya maombi **Tsh. 20,000/=**

## 11. Baada ya Kuwasilisha Maombi

- Ukaguzi wa ghala linaloombewa leseni na Afisa wa Bodi
- Kuweka **Kinga ya Utendaji** kwa kuzingatia masharti yatakayoainishwa baada ya maombi kuwasilishwa Bodi
- Endapo wafanyakazi hawana mafunzo ya WRRB watapaswa kushiriki, kufanya mtihani na kufaulu

# Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Kuwasilisha Maombi ya Leseni ya Meneja Dhamana

Kujaza **Fomu Namba 9** na kuwasilisha viambatisho muhimu kama vilivyoanishwa hapo chini

## 1. Nyaraka za Kampuni

- Nyaraka za usajili kutoka mamlaka husika;
- Makubaliano ya Wakurugenzi wa Kampuni inayoomba leseni kufanya biashara inayoombwa kwenye ghala husika sambamba na utayari wa kulipa ada, kuwa na kinga ya utendaji na kufanya kazi kwa mujibu wa viwango vinavyotolewa na Bodi;
- Picha za Wakurugenzi/Wanahisa zilizothibitishwa na Mwanasheria;
- Wasifu wa Wakurugenzi/Wanahisa uliothibitishwa na wanasheria;
- Mchoro wa ramani unaonesha mahala makao makuu ya ofisi za Mwombaji zilipo au kuainisha namba za longitudi na latitudi;
- Leseni ya biashara ya eneo/wilaya husika

## 2. Taarifa zinazohusu Masuala ya Fedha;

- Barua ya uthibitisho wa akaunti ya Kampuni kutoka benki husika;
- Taarifa za fedha za Kampuni za karibuni;

## 3. Taarifa za Wafanyakazi Muhimu;

- Vyeti vya taaluma;
- Vyeti vya taaluma maalum (professional certificate);
- Leseni
- Wasifu wa wafanyakazi;

## 4. Gharama za maombi

- Mwombaji atalipa ada ya maombi **Tsh. 20,000/=**;
- Ada ya Leseni **Tsh. 200,000/=** kwa mwaka.

## 5. Uthibitisho wa Mafunzo Maalum ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Wafanyakazi

- Mafunzo ya Meneja Dhamana au;
- Mafunzo ya Soko au,
- Mafunzo ya Uwezeshaji Fedha Vijijini